# The Foundation News

ISSN 1821-5335 | Jarida la The Foundation for Civil Society | Oktoba - Disemba, 2006


# Asasi za Kiraia: Uwezo Wa Kiutendaji Haujaimarika - Utafiti



## Ndani ya Toleo







# Ujumbe Kutoka kwa Mkurugenzi


**"The Foundation News" ni jarida linalotolewa na The Foundation for Civil Society kwa lengo la kupashana habari juu ya shughuli zake na zile za sekta ya jumuiya za kiraia Tanzania.**

**Mchapishaji**
The Foundation for Civil Society

**Mhariri**
Joseph Mzinga

**Kamati ya Uhariri**
Deogratius Mlay
Peter Sitta
January Basela
Rehema Shija

**Usanifu**
PENplus Limited
+255 22 2182059
design@penplus.co.tz

**Kwa mawasiliano:**
The Foundation for Civil Society
Haidery Plaza, Ghorofa ya tano,
Mtaa wa Upanga/Kisutu
S.L.P. 7192, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2138530/1/2
**Faksi:** +255 22 2138533
**Barua pepe:** information@thefoundation-tz.org



Maoni yaliyotolewa na wachangiaji siyo lazima yanawakilisha mtazamo wa the Foundation for Civil Society au Wabia wake wa Maendeleo. Mchapaji amechukua hadhari kuhakikisha usahihi wa taarifa zote na hawajibiki kwa tatizo lolote litakalotokana na makosa yaliyofanywa kwa nia njema katika chapisho hili.


**Kwa mara nyingine tena mwaka 2006 unamalizika kama mwaka wa mafanikio kwa sekta ya asasi za kiraia (AZAKi) nchini. Sekta hii imeendelea kutekeleza majukumu yake katika jamii ikiwa ni pamoja na kutoa huduma kwa jamii, kufuatilia mwenendo wa sekta nyingine za kijamii na kutoa elimu juu ya sera, sheria na haki kwa jamii na makundi mbalimbali. Ni matumaini yangu kuwa tunauangalia mwaka mpya unaokuja tukiwa tumejiweka tayari kufanya mambo mengine makubwa zaidi kwa maendeleo ya taifa letu.**

Kwa upande wa the Foundation, tunaona mwaka 2006 kuwa mwaka mwingine wa mafanikio. Tangu siku ya kwanza ya mwaka huu, tulijipangia malengo yetu na kuweka viashiria vya harakati zetu. Lengo letu lilikuwa kuimarisha uwezo wa AZAKi ili ziweze kujenga jamii ya watanzania wenye kuelewa wajibu na haki zao katika maendeleo.



julanga@thefoundation-tz.org

Shughuli zetu zilijikita katika utoaji wa ruzuku na kujengea uwezo AZAKi. Kwa kipindi cha mwaka 2006 tumetoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 6.6 kwa asasi za kiraia 352. Aidha tumesaidia ujenzi wa uwezo wa asasi za kiraia kupitia mafunzo ya aina mbalimbali: Wajibu wa kijamii wa sekta ya biashara (corporate social responsibility), bajeti ya kijinsia; hatua za bajeti za umma na ufuatiliaji wake na hali kadhalika mafunzo ya namna ya kusimamia fedha na kuimarisha mashirika (organisational development).

Kwa kipindi cha mwaka huu pia tumefanya mikutano na wadau mbalimbali kwa ajili ya kujifunza, kupanga mikakati na kutandaa

**inaendelea uk. 1**

## Tahariri

**Mpendwa msomaji wetu, kwa mara nyingine tena tunasema asante kwa kutuunga mkono na kutupa mrejesho juu ya jarida lililopita. Toleo hilo limehamasisha maoni, na ushauri kutoka kwenu kwa ajili ya kuboresha toleo hili na yajayo. Tunaheshimu mawazo na maoni yenu. Yana maana ya pekee na tunayazingatia. Endeleeni kutuletea maoni, tutayapokea na kuyafanyia kazi. Tunatambua kuwa safari kuelekea kwenye mafanikio ni ndefu. Mawazo yenu ndiyo dira pekee itakayotuwezesha tusipotee njia!**

Katika jarida hili la toleo la tatu, tuna habari mchangayiko. Toleo hili limeandika pia barua zenu zilizotufikia. Katika barua hizo mmependekeza kuwa *the Foundation News* ikaribishe habari kutoka kwa washirika wengine wa maendeleo. Tumelipokea hilo. Na katika jarida hili tuna matokeo ya utafiti wa Shrika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kuhusu uwezo wa kiutendaji wa asasi za kiraia - AZAKi. Makala hii inatoa mwangaza kwa ufupi kuhusu changamoto za kiutendaji zinazokabiri asasi nyingi za kiraia nchini.



mzinga@thefoundation-tz.org

Midahalo ni njia ya kujenga uelewa mmoja wa pamoja, hukuza kufahamiana na ubia wa kimaendeleo. Ndiyo maana tuna habari

**inaendelea uk. 3**

# Yaliyomo

2



7



11



18




Barua Kutoka kwa Wasomaji Wetu ........ 1
Uwezo Duni wa Kiutendaji Unakwamisha Maendeleo ya AZAKi ........ 2
The Foundation Kutathmini Mitandao ya AZAKi ........ 3
Tuzungumzie Mitandao ya AZAKi ........ 4
Awamu ya Tatu ya Ukaguzi na Upimaji wa Mafanikio ya Wafadhiliwa Yaanza ........ 5
Wawakilishi wa Asasi za Kiraia 183 Wapata Mafunzo ........ 7
Ulingo wa Maendeleo Shinyanga ........ 9
Sekta ya Biashara Iwajibike Kuleta Maendeleo yaJamii ........ 10
Maonesho katika Baraza la Wawakilishi Kufanyika Aprili ........ 11
Shirika dogo laibuka na mkakati wa kuhakikisha haki za wasafiri ........ 12
AZAKi Morogoro Zapania Kuimarisha Mawasiliano ........ 13
Fomu, Mwongozo wa Maombi ya Ruzuku Sasa Kwenye Mtandao ........ 15
Mjue Mwamuzi wa Maombi Yako ya Ruzuku ........ 16
Orodha ya Asasi Zilizopata Ruzuku - Oktoba 2006 ........ 18
Wadau wasaini MoU Kusaidia Foundation ........ 23


# Ujumbe Kutoka kwa Mkurugenzi

**inatoka ukurasa wa uhariri**

(networking). Mwezi Mei tulikutana na mitandao ya AZAKi ambapo misingi ya namna ya kufanya kazi ilijadiliwa. Mwezi Aprili tuliweza kuandaa maonesho ya AZAKi Bungeni Dodoma kwa kushirikiana na SUNY Tanzania na ofisi za Bunge. Wawakilishi wa AZAKi wapatao 130 kutoka mikoa 18 walihudhuria. Katika maonesho hayo wabunge 240 walitembelea maonesho hayo ambapo walibadilishana mawazo na uzoefu na wawakilishi wa AZAKi kuhusu mambo ya sera na sheria. Vile vile, mwezi Agosti tuliandaa tamasha na maonesho ya kila mwaka ya AZAKi. Tamasha hilo lilifunguliwa na Makamu wa Rais Dk. Ali Mohamed Shein, na kushirikisha washiriki wapatao 600 katika kujadili dhima ya AZAKi katika mapambano dhidi ya rushwa.

Katika kipindi chote cha mwaka, tumewezesha pia, kwa ubia, midahalo ya ulingo wa maendeleo katika mikoa 17 nchini ambapo watu wapatao 2,000 walipata fursa kujadili Mkakati wa taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA). Pia tuliweza kukusanya, kutangaza na kusambaza habari mbalimbali kuhusu AZAKi kupitia vyombo vya habari vya magazeti na redio. Na zaidi tuliweza kuanzisha jarida hili "the Foundation News".

Tunapotafakari na kupanga mikakati ya 2007, tunapenda kuwashukuru wale wote waliotusaidia kwa namna moja au nyingine. Tunatambua kuwa *mafanikio siyo matokeo ya bahati njema bali ni uchaguzi na mipango madhubuti; mafanikio siyo kitu cha kukingojea bali huja kwa kufanyiwa kazi!*

Tunawatakia mwaka mpya wenye mafanikio

**John Ulanga**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**the Foundation for Civil Society**

# Jarida litoe nafasi kwa habari za wadau mbalimbali

Tunakuarifu kupokea nakala mbili za jarida la "The Foundation News". Jarida hili ni la kiwango cha hali juu na mambo mengi yameandikwa kwa uwazi na linazungumzia masuala mbalimbali ya muhimu kwa AZAKi. Ni vyema wadau mbalimbali waandike habari juu ya nini wanafanya huko waliko, pia tunaomba kupatiwa nakala zaidi za jarida kwani tunafanyakazi na AZAKi 26 na nakala mlizotuletea ni mbili tu.

**Stephen Banda**
SOPF-Songea

*Bwana Banda, asante kwa maoni yako. Katika safu ya Tahariri nimekuwa nikiomba mtutumie taarifa zenu nasi tunaahidi tutazichapisha* – **Mhariri**

# Nimefurahishwa na Tamasha la Jumuiya za Kiraia

Nimefurahi kupokea nakala ya jarida la "The Foundation News" na kwa kuwa nilishiriki katika Tamasha la siku mbili la Asasi za Kiraia pale kwenye viwanja vya Karimjee mwezi Agosti 2006, ninaweza kuhusisha kwa urahisi kile ambacho sasa nakiona kwenye jarida. Tutashukuru kupata nakala zaidi za Jarida hilo. FOGOTA ina vikundi vya washirika 24 katika mikoa minne; kwa hivyo tunahitaji nakala zaidi.

**Emmanuel Kazungu**
Forum for Grassroot Organisations Tanzania (FOGOTA)

# Habari safi

Tumepokea nakala mbili za jarida "The Foundation News". Asante sana kwa nakala hizo. Hata hivyo tunaomba tupatiwe nakala nyingi zaidi ili tuweze kuzifikisha kwa wadau wetu katika wilaya zote za mkoa wa Lindi, kama inawezekana tunaomba nakala kati ya kumi na kumi na tano. Hongera kwa ushirikiano wenuu na huduma yenu kwa AZAKi nchini kote.

**Sharrif Maloya**
**LINGONET-Lindi**

# Tunahitaji nakala zaidi

Tunashukuru kupatia jarida la "The Foundation News", hata hivyo kwa kuwa shirika letu lina wanachama wengi ambao ni muhimu kujua mambo mbalimbali yanayofanywa na shirika lenu kwa ajili ya maendeleo ya jamii yetu. Tunakuomba kupatiwa majarida mengi zaidi.

**Alatanga Nyagawa**
**NJODINGO-Njombe**

# Zaidi.....

Tunakiri kupokea nakala za toleo la pili la Julai hadi Septemba la "The Foundation News". Lakini hata hivyo tunapenda tupatiwe nakala sitini zaidi kwa ajili ya kuzitawanya kwa AZAKi, na mitandao mbalimbali ya wilaya hapa mkoani Rukwa.

**Stanley Mshana**
**RANGO-Sumbawanga**

*Ndugu Kazungu, Mshana, Maloya na Nyagawa, The Foundation itaangalia uwezekano wa kuchapisha na kusambaza nakala zaidi-* ***Mhariri***

# Punguzeni picha

Kwa wingi wa heshima tunapenda kukuarifu kuwa tumekuwa tukipokea kutoka the Foundation majarida kwa mara ya tatu sasa, na kimsingi tunajifunza mambo mbalimbali yanayotekelezwa na the Foundation. Hata hivyo tunashauri picha zipungue jarida na badala yake habari ziongezwe; pia tungependa jarida liwe na habari zinazohusu matatizo na mafaniko ya AZAKi mbalimbali.

Pia tunahitaji kufahamu ikiwa wanaotaka kuandika habari muhimu kutoka kwa wadau wa FCS wanarudishiwa gharama zozote za kufidia matumizi yao.

**Abdalla Mmanga**
**Jumuiya ya UHAI-Zanzibar**

*Bwana Abdalla, asante kwa maoni yako. Juu ya kurudisha gharama, tunafikiria utaratibu wa kufidia kiasi kidogo cha taarifa endapo kuna gharama zilizotumika katika kutafuta na kuandika makala. –* ***Mhariri***





# Uwezo Duni wa Kiutendaji Unakwamisha Maendeleo ya AZAKi - Utafiti

Na Zaa Twalangeti



zaajohn@yahoo.com

**Imeelezwa kuwa Asasi za Kiraia (AZAKi) nyingi hapa nchini zinashidwa kwenda sanjari na mchakato wa maendeleo kutokana na kutokuwa na uwezo na utendaji duni. Hayo yamebainishwa katika utafiti uliofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) juu ya uwezo wa AZAKi kushiriki kikamilifu katika michakato ya ya maendeleo katika ngazi ya serikali za mitaa. Utafiti huo uliendeshwa na Bwana Japhet Makongo kutoka taasisi ya Ubunifu.**

Hayo yalijitokeza katika semina ya siku tano iliyofanyika mjini Morogoro na kushirikisha wawakilishi wa AZAKi kutoka sehemu mbalimbali Tanzania. Semina hiyo ilikuwa inalenga kutoa mrejesho wa utafiti na kuzijengea uwezo AZAKi.

Matokeo hayo ambayo yalikuwa ya kutathmini hali ya AZAKi na uwezo wao katika kushiriki kwenye michakato ya maendeleo ya serikali za mitaani. Hatua hiyo ni ya kwanza kabla ya kuanza mchakato wa mradi wa TANGO na UNDP ambao unalenga kuboresha ushiriki wa AZAKi katika mchakato wa maendeleo katika serikali za mitaa. Hata hivyo utafiti ulibaini kuwa ni AZAKi chache ambazo zina uwezo unaotakiwa kufanya uchambuzi tunduizi wa kina wa sera. Hali hiyo inazifanya AZAKi nyingi zinashindwa kwenda sambamba na mchakato wa kufanya uchambuzi wa sera, ufuatiliaji wake na pengine kushiriki katika kuziandaa.

"Changamoto nyingine ni uwezo mdogo wa kiufundi wa AZAKi katika kufanya tafiti kabla ya kufanya kazi zao za ushawishi, utetezi au ufuatiliaji. Hali hii imefanya hoja zaokutochukuliwa kwa uzito unaostahiri na Serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo," alieleza Bw. Makongo

"Hata wakitaka kujenga hoja, kupinga au kufafanua, wawakilishi wa AZAKi za Tanzania hushindwa kufanya hivyo kutokana na kuwa na mbinu duni za kufanya ushawishi na utetezi," alidai Bw Makongo.

Katika kupima hoja za matokeo ya utafiti wake ulionyesha kuwa AZAKi nyingi hazina mipango ya kimkakati ya muda mrefu ya kufanya ushawishi na utetezi, Bw. Makongo aliwataka washiriki wa semina hiyo kubainisha mikakati ya utetezi wa AZAKi zao, kati ya washiriki 40 ni watatu waliweza kuelezea walau kuelezea kuwepo kwa mpango mkakati wa utetezi katika taasisi zao. Hali hii inaonyesha kuwa asasi nyingi hazina mipango ya utetezi na hurukia ajenda bila mpangilio maalumu.

Vile vile ilibainika kuwa uwezo mdogo wa ufahamu na kukosekana kwa mifumo madhubuti ya mawasiliano kumesababisha kutokuwepo kwa mawasiliano kati ya AZAKi na wanachama na walengwa wao.

"AZAKi za Tanzania zimejikita katika kutekeleza masuala mengi ya kimaendeleo, lakini hata hivyo mchango wake haujulikani vilivyo kwasababu ya kukosa mikakati ya kuandika na kusambaza machapisho yanayohusu kazi zao," alibainisha mtafiti huyo.

Akielezea matatizo ya kiutendaji wa AZAKi, Makongo anasema, "AZAKi katika ngazi za msingi hazina dira (vision) na malengo (mission) ambayo yanaeleweka bayanajambo ambalo linawafanya wanajamii wa maeneo ambayo AZAKi hizo zinafanyia kazi kushindwa kujitambulisha na malengo ya AZAKi husika," Tatizo hilo kwa mujibu wa Makongo linatokana na AZAKi kushindwa kusimamia dira na malengo yake kwa umahiri.

**inaendelea uk. 4**

## Tahariri

*kutoka ukurasa wa Tahariri*

kuhusu mdahalo wa ulingo wa maendeleo mkoani Shinyanga. Aidha habari juu ya mafunzo mbalimbali yaliyoandaliwa au kufadhiliwa na the Foundation ikiwemo ile ya wajibu wa sekta ya biashara katika maendeleo ya jamii (corporate social responsibility) zimo ndani ya toleo hili.

Aidha tunazo habari mbalimbali juu ya matukio yajayo. Haya ni pamoja na maonesho ya AZAKi katika Baraza la Wawakilishi mwezi Aprili huko mjini Zanzibar, utafiti utakaofanyika kuhusu hali ya mitandao ya AZAKi na tathmini ya mashirika wafadhiliwa na the Foundation. Pia kama ilivyo desturi tunazo kurasa mahsusi zinazojulikana kama kona ya ruzuku kukuhabarisha juu ya huduma yetu hiyo.

Nakutakia usomaji mwema

**Joseph Mzinga**
**Mhariri**

# Uwezo Duni wa Kiutendaji Unakwamisha Maendeleo...

*inatoka uk. 2*

Tatizo la kushindwa kuwa na mitandao imara ya AZAKi ni jambo jingine ambalo lilidhihirika katika utafiuti huo. Eneo hilo linahitaji kuboresha ili kuziwezesha asasi za kiraia kutimiza wajibu wake ipasavyo. Hali hii inadhihilika kutokana na ukweli kuwa licha ya kuwepo kwa mitandao mingi ya AZAKi katika ngazi za wilaya na mikoa bado asasi za kiraia hazijaweza kutumia kikamilifu uwepo wa mitandao hiyo kwa ajili ya kuimarisha mshikamano miongoni mwao. "Imedhihirika kuwa sekta ya asasi za kiraia inafanya kazi katika mafungu mafungu", alisema mtafiti huyo. "tatizo lingine kubwa ni juu ya mahusiano, hakuna kuaminiana kwa kutosha kati ya serikali za mitaa na asasi za kiraia; hivyo ni vigumu sana kwa vyombo hivi viwili kujenga ubia wa kuaminiana", alisema Bw. Makongo.

Aidha utafiti huo ulibainisha kuwa suala la uwajibikaji kwa wananchi na walengwa miongoni mwa AZAKi bado linahitaji kufanyiwa kazi na kusema "utafiti unaonesha kuwa asasi za kiraia zinawajibika zaidi kwa serikali na wafadhili kuliko kwa jamii walengwa na matatizo yao; kwa kuwa ni wazi kuwa jamii hizo ndiyo wanaozifanya asasi za kiraia kuwa na sababu ya kuanzishwa".

Kuhusu uwezo wa kukusanya na kutumia rasilimali, utafiti huo ulionyesha kuwa asasi nyingi katika ngazi za wilaya na mikoa hazina uwezo mkubwa wa rasilimali watu na rasilimali fedha hivyo kuhatarisha uendelevu wake.

Kutokana na matokeo hayo ya utafiti, TANGO na UNDP wameandaa mikakati ya kuhakikisha matatizo hayo ya AZAKi yanafanyiwa kazi. Mikakati hiyo ni ya muda mrefu na muda mfupi.

Moja ya mikakati ya muda mrefu ni kusaidia kuimarisha ujuzi wa AZAKI katika kufuatilia bajeti za serikali katika ngazi ya wilaya na taifa. Miongoni mwa mikakati ya muda mrefu ni pamoja na kusaidia uwepo wa mitandao imara ya AZAKi katika ngazi zote.

Mikakati ya muda wa kati ni pamoja na kuboresha njia za mawasiliano kwa kuwezesha kuwepo kwa vituo vya habari katika kila wilaya, kuboresha mahusiano kati ya AZAKi na serikali za mitaa kupitia midahalo.



*Majadiliano ya vikundi ni njia moja ya kukuza uwezo wa AZAKi*

## Capacity Assessment of Civil Society Organizations in Tanzania

- **Policy analysis:** Very few CSOs have the skills needed to undertaken comprehensive policy analysis there for fail to follow through the government's policy making process.
- **Research:** Like the issues of policy analysis most CSOs lack the skills needed for undertaking research which can be taken to be credible by government and other development actors.
- **Programming and Planning**: Most CSOs in Tanzania do not have well defined strategic plans and therefore undertake adhoc advocacy activities which are not ground rooted.
- **Communication and information:** Most CSO have very poor information and communication systems and therefore fail to reach their constituencies in time when soliciting information or giving feedback on the various development process.
- **Advocacy skills:** Even when they have an issue to put across Tanzanian CSOs do not have the skills needed for effective advocacy.
- **Documentation:** CSOs in Tanzania engage in a number of development processes; however their impact is not felt due to poor documentation and information packaging.
- **Regarding the issue of functional capacities the following was observed:**
- **Vision and Mission:** It was noted that most CSO do not have very clear visions and missions. Meaning that the community or the people they purport to serve do not identify with the work they are doing or the CSO fails to leave by its vision and mission.
- **Relationship:** the workshop noted that despite the recent increase in the number of district and regional NGO networks still CSO in the country have not maximized the benefits brought about by networking and solidarity building. The CSO sector is still seen as working in separate pockets.
- **Accountability:** The accountability of CSOs in Tanzania is lopsided in that they are more accountable to government and the donors, than they are to their constituencies who are the reason why the CSOs exist.
- **Human and financial resources:** Most CSOs do not have adequate human resources, this problem is compounded by the fact that most people working in CSOs sector are not every competent. Further the study established that very few CSOs have a sustainable funding base.
- **Mindset:** There is gross mistrust between government and CSOs at all levels national and sub-national levels therefore it is difficult to building effective partnerships.

# The Foundation kutathmini mitandao ya AZAKI

Na Deogratius Mlay




**MAANDALIZI ya kufanya utafiti juu ya hali ya mitandao ya asasi za kiraia (AZAKI) nchini yanafanyika ili kuiwezesha the Foundation for Civil Society na wadau wengine kupata `picha' halisi ya mitandao hiyo ili kushirikiana nayo kuimarisha ufanisi zaidi katika michakato ya maendeleo.** Utafiti huo unatarajiwa kuanza mapema mwanzoni mwa mwaka ujao.

Mkakati wa kufanya utafiti huo umefikiwa baada ya kubaini kuwa mitandao ya AZAKi ina mwanya mkubwa wa kukabiliana na matatizo mbalimbali kama vile kurudia miradi katika eneo moja na uhaba wa mzunguko wa taarifa miongoni mwa washiriki katika sekta ya kiraia.

Lengo kubwa la utafiti ni kutathmini uwezo wa mitandao ya AZAKi na wanachama wake ili kuibua mbinu za kuiimarisha, na hivyo kuziwezesha kuongeza ushiriki wa wananchi katika mchakato wa maendeleo.

Pamoja na mengine, maeneo ya utafiti huo yatakuwa ni kutathmini hali ya mitandao ya asasi za kiraia nchini tangu mwaka 2000 na malengo ya kuwepo kwake, uchanganuzi wa madaraka ya mitandao, uhusiano na wanachama wake na upembuzi juu ya ushiriki katika mijadala ya sera/maendeleo. Maeneo mengine ni kuchunguza kiwango cha ushirikiano wa AZAKi hizo na serikali, viongozi, wawakilishi waliochaguliwa na wananchi wakiwemo wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Vilevile, utafiti utapembua masuala nyeti ambayo yanahitaji kujengewa uwezo na kuendelezwa, mambo yaliyoanzishwa na wadau wengine kwa lengo la kuzisaidia AZAKi na namna ambavyo the Foundation inaweza kuimarisha ubia na mitandao iliyopo ili kupanua huduma zake hadi kwenye jumuiya za ngazi ya chini.

Maandalizi ya kufanya utafiti huo yameambatana na kuundwa kwa kamati ndogo ya ushauri. Kamati hiyo ina wawakilishi kutoka mitandao miavuli ya asasi za kiraia ikiwemo TANGO na TACOSODE, mashirika mengi yanayotoa mafunzo kwa AZAKi; PACT Tanzania, SNV, DEED na Baraza la AZISE. Wawakilishi wengine wanatoka katika Kitengo cha Uratibu wa AZISE na idara nyingine za serikali.



*Baadhi ya wawakilishi wa mitandao ya AZAKi nchini wakiwa katika majadiliano*

# Tuzungumze Mitandao ya AZAKi

Na Deogratius Mlay

**Mtandao ya AZAKi ni nini?**
Mtandao ni kundi lolote la asasi za kiraia ambao kwa azma zao wenyewe, wanaamua kubadilishana habari au kufanya kazi pamoja. Hata hivyo ushirikiano huo jhauwafanyi wapoteze utambulisho wa mashirika yao.

**Mitandao ni nini?**
- Mitandao inajumuisha asasi moja moja au muungano wa mashirika ambao wana mkakati wa kubadilishana taarifa, mawazo, mbinu na kutumia rasilimali pamoja ili waweze kufikia lengo maalumu walilojiwekea.
- Mitandao huonyesha hali ya kuwa na tabia ya kushirikiana na siyo kuungana, huonekana katika ushirikiano wa watu, au kundi ambao kinachowaunganisha ni lengo la pamoja au kubadilishana habari au mbinu.
- Mitandao mingi huanzishwa ili kuboresha kubadilishana taarifa na habari miongoni mmwa wanachama. Lengo la msingi ni kubadilishana habari.

**Kutandaa (networking)**
- Kutandaa au networking hujumuisha kuwa na mawasilaino na kuhimiza ubadilishanaji wa taarifa na ubia katika mambo mbalimbali.
- Kutandaa ni mchakato wa kutafuta rasilimali na kuunganisha rasilimali zilizopo kwa lengo la kuongeza nguvu za pamoja kati ya asasi mbili au zaidi au kati ya mtandao na mtandao.

**Muungano (Coalition)**
Muungano uhusisha mashirika mawili au zaidi yanayoamua kufanya kazi kwa pamoja (au ushawishi) ili kufikia lengo walilojiwekea. Tofauti na mitandao, muungano au *koalisheni* huwa na mfumo wa utekelezaji au ufanyaji maamuzi ambapo wanachama wa muungano huwa na malengo ya muda mrefu kutumia kwa pamoja rasilimali na kutekeleza shughuli kuelekea kwenye lengo la pamoja. Mikakati ya *koalisheni* ni kitu cha muhimu katika ushawishi na utetezi.

**Ubia (Alliance)**
Ubia ni ushirikiano wa muda mfupi kati ya asasi mbili au zaidi. Huwa na lengo mahsusi la ubia.

**Nini Changamoto zinazokumba mitandao?**
1. mitandao mingi nchini haina lengo linalkoeleweka,
2. mitandao ina wanachama wa aina mbalimbali ambapo ni vigumu kufikia suluhu au uelewa wa pamoja. Aidha baadhi yao hupenda kuwa na sauti kubwa inayowakatisha tamaa baadi ya washirika.
3. mitandao mingi hutawaliwa na wanachama wachache au shirika linalotoa ofisi kwa ajili ya mtandao.
4. mitandao mingi haina fedha au rasilimali zingine muhimu
5. endapo fedha zipo, badi matatizo na kutoelewana huzuka



*Wawakilishi wa mashirika ya kutetea haki za afya (Health Equity) wakizungumza na Wawakilishi wa Wananchi mjini Dodoma*

# Awamu ya Tatu ya Ukaguzi Na Upimaji Wa Mafanikio Ya Wafadhiliwa Yaanza

Na Marilyn Elinewinga



marilyn@thefoundation-tz.org

**The Foundation for Civil Society inatarajia kuendesha ukaguzi na utafiti ili kupima matokeo na mafanikio yaliyopatikana kwa jamii kutokana na miradi iliyoifadhili.**

Zaidi ya mashirika 120 yatahusishwa katika utafiti huo ambao utaendeshwa na timu binafsi ya kuanzia Februari 2007. Zoezi hilo litatoa mwanga wa namna gani malengo yaliyopangwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa the Foundation for Civil Society wa mwaka 2005-2008 yatafikiwa.

Hii ni mara ya tatu kwa the Foundation kuendesha ukaguzi na upimaji wa matokeo kwa miradi iliyoifadhili ambapo mara ya kwanza na ya pili, utafiti wa namna hiyo ulifanywa na kampuni ya Economic Development initiatives (EDI) Ltd kwa kipindi cha mwaka 2003 na 2005.

Mambo makuu yaliyodhihirika katika tafiti zilizopita ni kuwepo kwa pengo la kiuwezo miongoni mwa asasi za kiraia kuhusiana na usimamizi wa fedha, ubunifu na usimamizi wa miradi, ufuatiliaji na tathmini, utetezi na ushawishi, uendeshaji wa mashirika na utunishaji mifuko.

Utafiti unaofuata utalenga zaidi katika kuangalia matokeo ya ruzuku ya the Foundation kwa asasi za kiraia na katika kusaidia jamii ambamo asasi hizo zinatekeleza miradi.

Matokeo yanayopatikana kutokana na utafiti huo yamekuwa muhimu katika utendaji wa



*Wawakilishi wa AZAKi katika harakati za Ushawishi*

Foundation na yametumika katika kurekebisha mwelekeo wa the Foundation hususani katika kubuni programu mpya kulingana na mahitaji ya wafadhiliwa.

Programu mpya tano za moduli za mafunzo zilianza mwishoni mwa 2005. Mafunzo haya ni matokeo ya mapendekezo ya ripoti za ukaguzi na upimaji wa mafanikio uliopita. Moduli za mafunzo zilianzishwa ni pamoja na ile ya namna ya kubuni miradi, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini yake; uchambuzi wa sera; uendeshaji wa mashirika; utunushaji rasilimali na namna ya kujenga ubia kati ya sekta binafsi na jumuiya za kiraia.

Utafiti wa mwaka huu unatarajiwa kuonyesha mchango wa the Foundation katika kufanikisha Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA) na Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) na malengo ya milenia (MDGs).



*Wawakilishi wa AZAKi katika moja ya mafunzo ya kujengewa uwezo yaliyofanyika DSM*

# Wawakilishi Wa Asasi Za Kiraia 183 Wapata Mafunzo

• Ni katika nyanja za Utunzaji fedha, na Ubunifu na Usimamizi wa Miradi

Na Bernard Kindoli



bernard@thefoundation-tz.org

**Mameneja na maafisa wapatao sitini na wanane kutoka Asasi za Kiraia (AZAKi) 34 za Tanzania Bara na Visiwani, wamenufaika na mpango wa mafunzo mahsusi kulingana na mahitaji juu ya Miradi na Usimamizi wa Fedha yaliyoandaliwa na kufadhiliwa na the Foundation, Disemba mwaka jana.**

Mafunzo hayo ya siku tano yalifanyika jijini Dar es Salaam kati ya Desemba 10 na 15, 2006 ambapo 34 kati ya wawakilishi 68 wa AZAKi walishiriki katika mafunzo ya kubuni miradi, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini wakati 34 wengine walishiriki mafunzo ya usimamizi wa fedha.

Mafunzo hayo yalikuwa ni sehemu ya juhudi za the Foundation katika kuchangia kuimarisha ufanisi wa AZAKi kupitia mpango wa kuendeleza uwezo. Malengo ya jumla ilikuwa ni kuwapa uwezo wa kutekeleza majukumu yao kitaalamu na kwa ufanisi na kuwafanya wawe washiriki bora katika kutekeleza programu za maendeleo katika maeneo yao

Mpango huo uliwalenga maafisa mipango, waratibu na watunza hazina kutoka asasi zinazopata ruzuku kutoka Foundation kwa kuwa wana majukumu kuhimu katika kupanga na kusimamia miradi. Wawezeshaji wa mafunzo hayo (MS TCDC - Arusha na Global Associates Tanzania LTD – Dar es Salaam) waliwapongeza washiriki kwa ushirikiano waliouonyesha, uchapakazi wao na kiu ya kutaka kujifunza na kuwa na shauku ya kuonesha tofauti katika utendaji wa kazi zao.

Kwa upande wao, washiriki waliishukuru Foundation kwa kuandaa na kugharimia mafunzo hayo na kusema stadi walizojifunza zitakuwa na manufaa kwao binafsi na kwa mashirika yao pia.

Akifunga mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Foundation, Bw. John Ulanga alisema kuwa ni matarajio ya Foundation kwamba mashirika yaliyonufaika na mafunzo hayo yataboresha utendaji wao na hivyo kuchangia malengo ya the Foundation kuzisaidia AZAKi kushiriki kikamilisfu katika juhudi za kupunguza umasikini chini.

Wakati huohuo wawakilishi 69 wa AZAKi walipata mafunzo ya Stadi za Utunishaji Mfuko ambayo yaliandaliwa na kufadhiliwa na Foundation for Civil Society na kufanyika jijini Dar es Salaam kuanzia Desemba 11 hadi 16, 2006.

Mafunzo hayo yaliwezeshwa kwa pamoja na SEIDA na TACOSODE ambapo miongoni mwa mambo mengine, washiriki walifundishwa maana ya ukusanyaji wa raslimali, misingi ya utunishaji mfuko na njia na mbinu za utunishaji mfuko. Malengo ya mafunzo yalikuwa yalikuwa ni kuwawezesha washiriki kufikiri, kubadilishana ujuzi, kujadili na kujifunza mbinu endelevu za utunishaji mifuko ili kugundua njia mbadala za kupata fedha kwa ajili ya kuimarisha malengo ya mashirika yao.

Mafunzo hayo yamelenga kujenga uwezo wa asasi za kiraia kupata fedha kutoka sehemu zingine mbalimbali ili ziweze kuwa endelevu kifedha na hivyo kupunguza utegemezi wa wafadhili.



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo wakimsikiliza Bwana John Ulanga, Mkurugenzi Mtendaji wa the Foundation.*

# Ulingo wa Maendeleo Shinyanga,

## • Makampuni makubwa yatakiwa kuchangia mchango
## • Wataka chuo cha ualimu.

Na Bernadeta Gambishi



shingonet2006@yahoo.com

**Shinyanga - Washiriki wa mdahalo wa ulingo wa maendeleo mkoani Shinyanga kuhusu Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini - MKUKUTA wametoa wito kwa makampuni makubwa yanayochimba madini mkoani humo kuchangia shughuli za maendeleo badala kutoa misaada midogo midogo. Mkoa wa Shinyanga ni moja ya mikoa ya Tanzania iliyojaliwa kuwa na madini mengi ya almasi na dhahabu.**

Wakizungumza katika mdahalo huo, washiriki wengi walionyesha kutoridhishwa na mwenendo wa makampuni makubwa yanayochimba madini mkoani humo; kuwa licha ya faida kubwa inayopatikana yamekuwa yakitoa vitu vidogo vidogo kwa jamii na taasisi za mkoani humo. Walivitaja vitu hivyo kuwa ni pamoja na vyandarua, vyakula na nguo ambavyo walisema kizazi kijacho hakitawaelewa kuona mashimo yaliyoachwa baada ya madini kuisha na faida ambayo madini hayo yameleta kwa mkoa.

Wachangiaji Abeli Seni, Tausi Nchenye, Agnes Makambajeki wamesema mkoa wa Shinyanga unahitaji miundo mbinu ya uhakika yakiwemo mabarabara, hospitali, na shule. Ambavyo wamesema makampuni makubwa ya uchimbaji madini yanaweza kusaidia ujenzi wake badala ya kutoa misaada midogo midogo.

Mdahalo huo uliwakutanisha zaidi ya washiriki 100 kutoka katika wilaya sita za mkoa wa Shinyanga na mikoa ya jirani. Uliandaliwa kwa pamoja na mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali mkoani Shinyanga – SHINGONET- na kufadhiliwa na the Foundation for Civil Society. Miongoni mwa washiriki waliohudhuria ni pamoja na wabunge wastaafu wa mkoa huo, naibu meya wa manispaa ya Shinyanga, madiwani, wanafunzi, watu wenye ulemavu na ambao wanaishi na virusi vinavyosababisha ukimwi.

Awali akiwasilisha mada mtaalamu kutoka sekretarieti ya Mkoa alitaja makapuni yanayochimba madini mkoani Shinyanga kuwa ni kampuni ya Williamson Diamonds (almasi) Kahama Mining Corporation (dhahabu) na E.L.Hilal Minerals Limited (almasi – Buganika). Aidha alisema hivi sasa faida inayolipwa serikali kutoka kwa makampuni hayo hupelekwa kwenye mfuko wa hazina makao makuu.

Wakizungumza jinsi ya kuimarisha sekta ya elimu mkoani humo, washiriki wa mdahalo huo walionyesha wasiwasi wa uwiano mbaya wa walimu na shule zilizopo. Mmoja wa washiriki Bwana Paschal Kilagula kutoka Tabora alisema Tanzania ina walimu wengi wasiofundisha. Alisema wengi wa walimu hao kwa sasa wamekimbia fani hiyo na wapo katika bunge, sekta nyingine za umma na binafsi. Bwana Kilagula alisema endapo mazingira ya walimu na maslahi yao yataboreshwa basi wengi watavutiwa kubaki katika fani hiyo ambayo alisema ina wahitimu wengi zaidi nchini. "Endapo tutakuwa na walimu wazuri, bado tunaweza kuzalisha wanafunzi bora hata kama tutakuwa na wanafunzi wanaosomea chini ya mti", alisema Bwana Kilagula na kushangiliwa na washiriki pamoja na watoa mada.

Aidha, washiriki pia walisema wakati umefika kwa mkoa wa Shinyanga kuwa na chuo cha ualimu, kwa kuwa ni mkoa huo ni pekee kwa Tanzania Bara usio na chuo cha ualimu. Washiriki walionyesha kushangazwa na hatua ya kubadilisha chuo cha SHYCOM kuwa shule ya sekondari na kuomba chuo hicho kibadilishwe tena kiwe chuo cha ualimu.

Mambo mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na afya husussani tatizo la UKIMWI, tatizo

**inaendelea uk. 12**



*Baadhi ya washiriki wa mdahalo wa Ulingo wa Maendeleo Shinyanga*

# Wadau wasaini MoU kuisaidia Foundation

Na Sitta Peter


sitta@thefoundation-tz.org

**WADAU watano kati ya nane waliioonesha nia ya kuisaidia asasi ya kiraia ya the Foundation for Civil Society wamesaini Hati ya Makubaliano (MoU) kuonesha azma ya kusaidia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa asasi hiyo kwa mwaka 2005 hadi 2008.**

Hati hiyo ilikubaliwa kwa pamoja kati ya the Foundation na wadau wanane wa maendeleo, ili itumike kama msingi wa makubaliano ya ufadhili kwa ajili ya kuisaidia Foundation.

Wadau waliosaini hati hiyo hadi mwishoni mwa 2006 ni Ubalozi wa Uholanzi (RNE), Wakala wa Maendeleo na Ushirikiano wa Uswisi (SDC), Ubalozi wa Denmark, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) na Ubalozi wa Ireland. Wadau wengine ambao ni Wakala wa Maendeleo wa Kimataifa wa Kanada (CIDA), Ubalozi wa Kifalme wa Norway na Ubalozi wa Kifalme wa Sweden wanatarajiwa kusaini hati hiyo mwaka 2007.

Hata hivyo wadau watatu walisaini makubaliano ya kuifadhili the Foundation baada ya kutekelezwa sharti la awali lililohusu kuwepo angalau wadau wawili kati ya wale waliosaini MoU ili kuruhusu utekelezwaji wa hati hiyo.

Wadau waliosaini makubaliano ya ufadhili na the Foundation ni Wakala wa Maendeleo na Ushirikiano wa Uswisi (SDC), Ubalozi wa Sweden na Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa wa Denmark (DANIDA).

SDC walikuwa wa kwanza kusaini makubaliano ya ufadhili wa Dola 2,076,923 za Kimarekani kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa shughuli za Foundation kwa miaka mitatu ambapo asasi hiyo itapokea Dola 690,000 kwa mwaka.

SDC ni miongoni mwa wafadhili wakuu wa the Foundation tangu kuanza shughuli zake mwaka 2003. Mwaka 2003, ilitoa ufadhili wa kifedha kiasi cha Dola 516,300 za Kimarekani, mwaka 2004 Dola 615,600, mwaka 2005 ilitoa Dola 1,000,000 na mwaka 2006 ilitoa Dola 200, 0000.

Ubalozi wa Sweden ulikuwa wa pili kwa kusaini makubaliano ya ufadhili wa Kronor za Sweden (SEK) 1,600,000 (sawa na Dola 220,000 za Kimarekani) ili kuisaidia the Foundation ambapo ilionesha kuridhishwa na huduma zinazotolewa na Foundation na azma yake katika kusaidia asasi za kiraia nchini Tanzania.

Jambo la kufurahisha na kushukuru ni kwa Ubalozi wa Denmark kupitia Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (DANIDA) kuungana na wadau wengine wa maendeleo katika kuisaidia the Foundaton ambapo Novemba 2006 ulisaini makubaliano ya msaada wa Dola 845,000 za Kimarekani kwa the Foundation, ikiwa ni mara ya kwanza kwa Foundation kupokea msaada kutoka ubalozi huo.

Ubalozi wa Denmark ulionesha nia ya kuisaidia the Foundation tangu mwaka 2005 wakati wa mashauriano na kundi la wadau wa maendeleo na mchakato wa kuandaa MoU ulipoanza. Muda wa utekelezaji wa ufadhili wa kifedha kutoka ubalozi huo ni kuanzia Oktoba 2006 hadi Disemba 2008 na fedha zote zitatolewa kwa mkupuo mmoja.

The Foundation ina matumaini ya kusaini makubaliano ya ufadhili zaidi na wadau wa maendeleo waliobaki na ambao wamesaini hati hiyo lakini hawajasaini makubaliano ya ufadhili. Gharama ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Foundation wa mwaka 2005-2008 zinatarajiwa kufikia Dola 30,279,000 za Kimarekani.



*Bwana John Ulanga, Paul Sherlock (DCI) na Anne Lucie Lefebvre (CIDA) katika moja ya mikutano kati ya the Foundation na Wabia wa Maendeleo.*

# Maonesho katika Baraza la Wawakilishi kufanyika Aprili

Na Sitta Peter

**WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wameandaliwa maonesho ya Asasi za Kiraia (AZAKi) yatakayofanyika wakati wa kikao cha Baraza hilo kitakachofanyika Aprili mwaka ujao.**

Maonesho yaliyoandaliwa na Foundation for Civil Society ni ya kwanza kufanyika kisiwani Zanzibar, na yamepangwa baada ya kuona mafanikio yaliyopatikana kwenye maonesho kama hayo yaliyofanyika mara mbili katika Bunge la Muungano mjini Dodoma, takribani miaka miwili iliyopita.

Maonesho ya kwanza yalifanyika Julai 2004 na yaliandaliwa kwa ushirikiano kati ya Foundation na Chuo Kikuu cha Kitaifa New York (SUNY) na kufadhiliwa na Wakala wa Kimaendeleo ya Kimataifa wa Marekani (USAID)-chini ya Mpango wa Ufadhili wa Kuimarisha Bunge na yalihudhuriwa na wabunge wapatao 200 na zaidi ya AZAKI 60.



*Maonesho ya AZAKi Bungeni Dodoma*

Maonesho yaliyofuata yalifanyika Aprili mwaka huu na kufadhiliwa na Foundation, SUNY Tanzania na ofisi za Bunge ambapo AZAKi 67 kutoka mikoa 16 ya Tanzania Bara na Visiwani zilishiriki, 50 kati ya hizo zilifadhiliwa na Foundation.

Mawasiliano rasmi na Baraza la Wawakilishi na AZAKi za Zanzibar zikiongozwa na ANGOZA na UWZ, ikiwa ni sehemu ya mchakato wa maandalizi yanafanyika. Jumla ya AZAKi 50 kutoka visiwa vyote vya Zanzibar zinatarajiwa kuhudhuria maonesho.



*Maonesho ya AZAKi Bungeni Dodoma*

Moja na maonesho, wawakilishi wa AZAKi watakutana na kujadiliana na kamati mbalimbali za Baraza, kujadili nyanja maalum wanazozifanyia kazi na ambazo zinahusiana na majukumu ya kamati husika.

Maonesho yanatarajiwa kutoa nafasi kwa wawakilishi wa AZAKi kupenyeza masuala yao ya ushawishi na utetezi kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazo ni pamoja na uwasilishaji wa taarifa, mihtasari ya sera na hadidu, taarifa za utafiti, video na vipeperushi na mabango.

# Waibuka na Mkakati wa Kulinda Haki za Wasafiri

Na Robert Mgeni


robert@thefoundation-tz.org

**Dar es salaam- Kuna mabadililiko makubwa ya mweleleo wa Asasi za Kiraia (AZAKi) nchini katika kubuni mbinu za kutatua matatizo ya jamii. Mathalani kuundwa kwa asasi inayotetea maslahi ya wasafiri nchini inayojulikana Campaign for Travelers Safety (CTS) linadhihirisha mweleleo mpya wa wanachamii kutaka kutatua matatizo sugu.**

Shirika hili baada ya kujaribu kupata ruzuku kutoka the Foundation kwa mara mbili, hatimaye lilifaulu kupata ruzuku ndogo mwaka 2006. licha ya uchanga na udogo wa ruzuku shirika hilo lenye makao yake jijini Dar es dalaam, lipo mstari wa mbele kutetea mabadiliko kuhusu haki za wasafiri

Mkurugenzi Mtendaji wa CTS Bw. Adam Msenga amesema katika kuhakikisha maslahi wa wasafiri yanalindwa mwezi Februari mwaka huu waliandaa semina ambayo iliwakutanisha wadau wote katika sekta ya usafirishaji wakiwemo viongozi wa askari wa usalama barabarani Bima, wizara, asasi za kiraia na taasisi za kimataifa.

"kwa kweli semina yetu ilifanikiwa sana kwani wadau wote katika sekta ya usafiri walikuwepo, tulikuwa na wawakilishi wa trafiki polisi kutoka Pwani, Dodoma, Morogoro na Kinondoni, pia kulikuwa na wawakilishi kutoka SUMATRA, BIMA, Wizara ya Afya, Wizara ya Miundombinu, Shirika la Afya ulimwenguni (WHO) na Kamati ya Usalama Barabarani, AZAKi na Shirika linalojihusisha na uuzaji wa mafuta - BP," alisema Bw. Msenga.

Mkurugenzi alisema kutokana na semina hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa Land Mark Jijini Dar es Salaam, CTS imefanikiwa kukubalika na wadau mbalimbali katika sekta ya usafiri.

Akizungumzia wiki ya usalama barabarani ya kimataifa ambayo kwa mara ya kwanza


Bwana Adam Msenga

inaazimishwa Aprili 13 hadi 29 kila mwaka, Bw. Msenga alisema kuwa asasi yake imeandaa semina maalum kwa shule nne za msingi ambazo wanafunzi wao wapo katika hatari ya kugongwa na magari.

Pia katika wiki hiyo, CTS kwa kushirikiana na WHO wamefanikisha safari ya mwanafunzi wa kidato cha nne kutoka Shule ya Sekondari Jitegemee, Cecilia Sintara kuhudhuria kongamano la ulimwengu juu ya usalama barabarani kwa vijana linalofanyika Jijini Geneva, Uswisi Aprili 23 hadi 27 mwaka huu.

Watu wengi na mali nyingi hupotea kutokana na ajali za barabarani.

Kuhusu mipango ya baadaye, Bwana Msenga amesema kuwa wanajiandaa kushawishi kuundwa kwa sheria inayomlinda msafiri kwa kuwa hadi sasa hakuna vipengele vinavyomlinda mtu anapokuwa safari dhidi ya matatizo yanayoweza kutokea. Aidha adha nyingine ni kuwepo kwa magari yasiyo na bima kama yale ya serikali ambayo baada ya ajali wahanga hupata matatizo makubwa ya kupata fidia.

Hii ni asasi ya aina yake kwa kuwa tumezoea kuona asasi nyingi zikijihusisha na masuala ya aina moja kama mazingira, magonjwa, watoto, Vijana na mambo ya Sheria. CTS wameonesha ubunifu ambao asasi zingine zinahitaji kujifunza na kuwa wabunifu katika kutatua matatizo ya jamii badala ya wote kukimbilia kufanya kazi za aina moja.

## Ulingo wa Maendeleo Shinyanga...

*inatoka uk. 9*

la maji na miundombinu, tatizo la mazingira, kilimo na utawala bora. Mambo hayo yote yalipangiwa mikakati wa ufuatiliaji kwa asasi za kiraia ukiongozwa na SHINGONET.

Jopo la wataalamu kutoka katika sekretatieti ya mkoa wa Shinyanga waliowasilisha mada katika mdahalo huo liliongozwa na ofisa mipango wa mkoa Bwana Ahmad Likoko. Wanajopo wengie walikuwa ni Mary T. Mashaka (kilimo), Charles Ng'atimwa, (misitu); James Sudi (madini) Injinia Deogratius Ntembeleha (maji); I.K Suluso (elimu); Raymond Kiwesa (afya) and Ahamad Likoko (utawala bora)

Mgeni rasmi katika mdahalo wa ulingo wa maendeleo alikuwa ni mkuu wa mkoa wa Shinyanga Brigedia mstaafu Dk. Balele aliyewakilishwa na Bi. Mwamvua Jilumbi.

# AZAKi Morogoro Zapania Kuimarisha Mawasiliano

## • Undugu, usiri na uongozi bora bado ni changamoto kwao

Na Venance Mlali, Morogoro




**Morogoro - Asasi za Kiraia mkoani Morogoro zimejengewa uwezo katika eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) lengo likiwa ni kurahisisha mawasilino kati ya mitandao ya wilaya mkoani hapa.**

Katika kuhakikisha kunakuwepo na mawasiliano ya uhakika kati ya AZAKi za kiwilaya shirika rafiki la HYVINKAA la Ufini limetoa simu za mkononi kwa mitanda ya AZAKi ya wilaya za Kilombero, Kilosa na Ulanga.

Pia UNGO ilifanikisha kupatiwa mafunzo ya TEKNOHAMA kwa baadhi ya wanachama wake lengo likiwa ni kuboresha ujuzi katika eneo hilo ambalo ni muhimu sana hususani kwa mawasiliano ya haraka na wadau wa ndani na nje ya nchi.

**Wakati huohuo** : Imeelezwa kuwa Asasi za kiraia ni kati ya nguzo moja muhimu katika maendeleo ya nchi, sekta nguzo nyingine ni sekta ya umma, serikali na sekta binafsi.

Asasi za kiraia ni muhimu kwani zinahakikisha kuwa viongozi wa Serikali wanatimiza majukumu yao ipasavyo na wanajibika kwa wananchi kwa kadiri ya ahadi zao.

Unapozungumiza AZAKi (Asasi za Kiraia) au AZISE (Asasi Zisizo za Kiserikali) unazungumzia sekta au nguzo moja kati ya tatu za maendeleo katika nchi. Pamoja nayo ni sekta ya umma au serikali na sekta binafsi. Sekta zote tatu zina nafasi ya pekee na muhimu katika kuleta maendeleo na ustawi wa kijamii na wa kitaifa.Kwa upande wa serikali,kazi kubwa iliyo nayo ni pamoja na kuhakikisha kuwa inatoa huduma za kijamii na kuboresha maisha ya wananchi wake, sekta binafsi inahakikisha kuwa inaimarisha uchumi wa nchi na azise zinahakikisha kuwa viongozi wa serikali wanatimiza majukumu yao ipasavyo na wanawajibika kwa wananchi.

AZAKi nyingi zikiwemo mitandao ya Kitaifa, kimkoa na wilaya zimefanya kazi kubwa sana katika kutekeleza majukumu yao. Asasi nyingi zilijikita katika kuwahamisha wananchi wanashiriki katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia masuala yahusuyo maendeleo yao.Hapa tunaona nafasi kubwa ya mitandao ya mikoa na wilaya katika kutimiza azma ya kuondoa umasikini nchini.

Zipo AZAKi zilizojikita katika kutoa elimu ya uraia, haki za binadamu, usawa wa kijinsia, kutafsiri Malengo ya Maendeleo ya Milenia na MKUKUTA ili kuwafikia wananchi na kufanya tafiti mbalimbali zenye kupelekea upunguzaji wa umaskini nchini. Zipo pia asasi zinazotoa huduma za kijamii kwa makundi mbalimbali katika kijamii.

Pamoja na kazi nzuri ya AZAKi hizo kuna changamoto ambazo hukutana nazo kila mara changamoto hizo ni pamoja na uwezo mdogo wa uendeshaji wa shirika; Mikanganyiko ya kiutendaji baina ya watendaji (wataalam walioajiriwa) na viongozi wa AZAKi hukosa ushirikiano kutoka kwa viongozi wa umma hasa wanapokuwa hawapo tayari kutoa taarifa zinazohusu matumizi ya fedha za umma.

Tatizo jingine kubwa ni kwa viongozi wengi wa AZISE kuwa katika mashirika mengi, hali hii husababisha kuwepo kwa udhaifu wa kiutendaji, kutokuwepo kwa ubunifu na moyo wa kujituma na ufanisi. AZISE nyingine huendeshwa kindugu, hapo mwanzilishi hayupo tayari kutoa nafasi sawa za watendaji wenye taaluma, badala yake hujikuta anabaki na ndugu zake wasio na ujuzi.


*Wawakilishi wa AZAKi wakifuatilia mafunzo ya kompyuta*

# Fomu, mwongozo wa maombi ya ruzuku sasa kwenye mtandao

Na Sunday Mtega

**KATIKA kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yake unakidhi matokeo ya kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA), the Foundation for Civil Society, imechukua hatua za makusudi kuimarisha tovuti yake kwa lengo la kufikisha taarifa za msingi kwa wadau wake kwa haraka zaidi. Tovuti hiyo ambao ni** www.thefoundation-tz.org umeshenehi taarifa zenye manufaa kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili.




*Washiriki wa Mdahalo wa Ulingo wa maendeleo mkoani Lindi wakiangalia fomu na mwongozo wa maombi ya ruzuku zinazotolewa na the Foundation*

Miongoni mwa taarifa hizo zinahusu fomu za maombi ya ruzuku na mwongozo kwa wadau wake, hasa waliopata ruzuku na wale wenye azma ya kuomba ruzuku kutoka the Foundation.

Awali, waombaji wa ruzuku walilazimika kuchukua fomu za maombi kutoka kwenye ofisi za the Foundation jijini Dar es Salaam, wakati wa mikutano ya upashanaji habari au kuomba kutumiwa kwa njia ya posta.

Hivi sasa waombaji wanaweza kupata fomu hizo kutoka kwenye mtandao huo kwenye maeneo yenye huduma ya mtandao wa mawasiliano, maarufu kama internet na hivyo kupunguza muda na gharama zilizokuwa zikitumika kuchukua fomu na kusambaza fomu kwa waombaji wa ruzuku.




*Bwana Sunday Mtenga, mtaalam wa Teknolojia ya Kompyuta wa the Foundation*

Aidha hazina ya data za mashirika wafadhiliwa zimewekwa katika tovuti ikiwa na taarifa za miradi iliyofadhiliwa, kiwango cha ufadhili, mahali ilipo na malengo yao, jambo ambalo litawawezesha wadau, husani asasi za kiraia, kubadilishana habari na uzoefu juu ya michango yao katika maendeleo ya jamii.

Pia, wasifu wa wafadhiliwa unatoa taarifa zaidi juu ya asasi mbalimbali za kiraia, idadi yake na kazi zinazofanya, taarifa ambazo zinaweza pia kutumika kwa malengo ya kuwa na mtandao na kushirikiana.

Kwenye tovuti pia kuna nyaraka na ripoti za the Foundation ikiwa ni pamoja na mipango na jarida pepe kwa waliojiandikisha.

Kutokana na maboresho hayo, tovuti ya the Foundation imemeweza kutembelewa na watu zaidi 20,000 ulimwenguni kwa takwimu za Disemba, 2006.

# Mjue Mwamuzi wa Maombi yako ya Ruzuku

Na Amon Mrutu


grants@thefoundation-tz.org

**Katika makala hii nimeona ni vema kuelezea utaratibu wa kupokea maombi mpaka pale maamuzi ya utoaji wa ruzuku yanapofanyika katika shirika letu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, kutojua mwenendo na mlolongo wa maombi ya ruzuku hadi kuidhinishwa kwake, limekuwa ni jambo linalotupa wakati mgumu na changamoto katika Idara ya Ruzuku ya Foundation.**

Mara nyingi kumekuwa na ugumu kuwaelimisha wateja ambao waliwahi kuleta maombi yao ya ruzuku kwa Foundation for Civil Society na kwa bahati mbaya yakashindwa kupitishwa na Kamati ya Uidhinishaji Ruzuku.

Tumekuwa tukikumbana na changamoto hiyo mara kwa mara, hasa kwa wateja wanaofika ofisini, wakati mwingine tunapokuwa kwenye mikutano na makongamano mbalimbali. Hii inatokana na kutoelewa vizuri jinsi uamuzi wa ruzuku unavyofikiwa.

Kuna baadhi ya waombaji wanaoamini kwamba wafanyakazi wa the Foundation wana uwezo wa kushawishi maombi yao yakapitishwa na Kamati ya Uidhinishaji hata kama hayana sifa zinazotakiwa. Kimsingi fikra hizo si za kweli hata kidogo.

Utaratibu wa kutoa Ruzuku katika Foundation for Civil Society ni wa wazi na unahusisha chombo huru ( Kamati ya Uidhinishaji) ambacho kuna wawakilishi mbalimbali kutoka AZISE, Serikali, vyama vya kitaaluma na vyuo vikuu.

Kamati hiyo inawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi wa the Foundation na wanafanya kazi zao kwa kufuata misingi maalumu inayoziwezesha asasi kupata ruzuku kwa uhalali. Wafanyakazi wa Foundation hawana uwezo wa kutoa maamuzi au kubadilisha uamuzi wa Kamati hiyo.

Kimsingi hatua ya kwanza ni mwombaji wa ruzuku kufikiria na kupata wazo la kuandika mradi katika eneo husika. Mwombaji anatakiwa kuchukua fomu na mwongozo wa maombi ya ruzuku ambazo zinapatikana katika ofisi za the Foundation jijini Dar es Salam na wawakilishi mikoani waliopo Mbeya, Singida ,Mtwara, Arusha na Zanzbari au kutoka kwenye tovuti ya Foundation.

Wakati wa kutayarisha andiko la mradi ni muhimu wanachama wa asasi wakashirikishwa ili kurahisisha wakati wa utekelezaji wa mradi na kupunguza migongano mara pesa za mradi zinapopatikana.

Baada ya kukamilisha andiko la mradi kwa kujaza fomu ya maombi, muombaji anatakiwa kuambatanisha vielelezo halali kama ilivyooneshwa kwenye muongozo wa mradi kutokana na aina ya ruzuku inayoombwa, huku akizingatia muda wa mwisho wa kuwasilisha maombi.

Mlolongo wa safari ya fomu ya maombi ya ruzuku huanzia pale inapowasilishwa na mwombaji katika ofisi za Foundation. Kila fomu inaorodheshwa na kupatiwa namba ya utambulisho mara tu inapo pokelewa.

Baada ya hapo hatua inayofuata ni mchakato wa fomu ya maombi kuanzia kwa maafisa wa the Foundation ambao huipitia na kuikagua kwa makini kuona kama muombaji ametimiza masharti yote na ameweka viambatanisho halali kama ilivyoelekezwa kwenye muongozo wa maombi ya ruzuku na kwenye fomu yenyewe.

Kabla ya kufanya kazi hiyo, maafisa wa the Foundation hutakiwa kujaza fomu ya kuthibitisha kutokuwa mahusiano binafsi na viongozi au shirika lililoomba ruzuku, (Declaration of Vested Interest). Maafisa hawa hutumia dodoso maalumu katika kupitia fomu za waombaji.

Zoezi la uchambuzi wa fomu za waombaji likikamilika, maombi ya miradi ambayo imetimiza vigezo vilivyoonyeshwa kwenye mwongozo wa ruzuku hupelekwa kwenye Kamati ya Uidhinishaji wa miradi kwa uchambuzi wa ngazi ya pili.

Kwa waombaji ambao hawakuweza kutimiza vigezo vilivyowekwa, huarifiwa kwa barua maalumu na wakielezwa sehemu zenye mapunguzfu na kuombwa kurekebisha na kutuma tena maombi.

Fomu za maombi zinazowasilishwa kwenye Kamati ya Uidhinishaji Ruzuku ni zile tu ambazo zimetimiza vigezo vilivyoorodheshwa kwenye muongozo wa uombaji ruzuku.

Kwa upande wake Kamati ya Uidhinishaji Ruzuku fomu za maombi hutumia dodoso maalumu ambalo linawawezesha kuona ubora wa miradi na kuonyesha kama shirika linaloomba ruzuku lina utawala bora na kama mradi utaleta matokea mazuri katika jamii.

Kabla fomu za maombi hazijakabidhiwa kwenye Kamati, Wajumbe wa Kamati pia hujaza fomu ya kuthibitisha kutokuwa na uhusiano binafsi na viongozi au shirika ambalo linaomba ruzuku, "Declaration of Vested Interest". Wajumbe wanapomaliza kazi ya kupitia fomu za maombi, huwasilisha taarifa katika kikao maalumu na kuzijadili taarifa za kila mradi ulioomba na uamuzi hufikiwa baada ya kupiga kura. Maombi yanayokubaliwa hupitishwa kwa kura nyingi.

Kwa miradi ambayo inapitishwa na kamati, utaratibu wa kusaini mikataba hufanyika na asasi husika hupatiwa ruzuku kama itakavyokuwa imekubaliwa katika mkataba. Uamuzi unaofanywa kwenye hatua hii huwa ni wa mwisho.

Hata hivyo kwa miradi ambayo itakuwa haikufanikiwa kupitishwa na Kamati ya Uidhinishaji, waombaji wanashauriwa kutuma tena maombi wakiwa wamefanya marekebisho ya mapungufu yaliyopo kwenye andiko la maradi wao na kuzingatia mwongozo wa Foundation kama itakavyokuwa imeelezwa kwenye barua ya majibu, ambayo itakuwa imeainisha mapungufu yaliyopo.

Kwa ujumla utaratibu wa kutoa ruzuku ni wa wazi unaozingatia maoni ya Kamati ya Uidhinishaji Ruzuku. Hakuna upendeleo wowote kwa mdau.

Kamati ndiyo yenye uamuzi wa mwisho na Maofisa wa Foundation hawana uwezo wa kuamua nani apewe au asipewe ruzuku. Ni haki ya kila mdau kupatiwa ruzuku endapo atakuwa ametimiza mashariti na kufuata taratibu za kutuma maombi kama ilivyo elekezwa kwenye muongozo wa uombaji ruzuku.

# Ruzuku ya Kati (MG) – Oktoba 2006

**Mnamo mwezi wa Oktoba 2006, kamati ya utezi ya the Foundation inayohusika na kuchagua asasi zinazofaulu kupata ruzuku imepitisha miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 2.045 kwa mashirika mbalimbali ya kiraia sitini. Yafuatayo ni majina ya asasi zilizopata ruzuku hiyo:**



rehema@thefoundation-tz.org

| Na | JINA LA SHIRIKA | MAELEZO YA MARADI KWA UFUPI | MKOA | KIASI KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Afri Art, P.O. Box 6073, Morogoro | Sensitize Community on how to implement law, rules and regulations of good governance. | Morogoro | 32,864,400.00 |
| 2 | Arusha NGO Network (ANGONET), P.O. Box 2388, Arusha | Enhance the capacity of District NGO Networks and CSO's of Arusha. | Arusha | 64,768,650.00 |
| 3 | Base for Education Dissemination, P.O. Box 6369, Mwanza | Capacity building to CSO's in Mwanza municipality. | Mwanza | 34,960,012.50 |
| 4 | Centre for Women and Children Development, P.O. Box 10740, Arusha | Provision of education on children's rights to stakeholders. | Arusha | 15,136,400.00 |
| 5 | Chama cha Viziwi Tanzania Tawi la Morogoro, P.O. Box 1776, Morogoro | Provide education on leadership and good governance to CHAVITA members in Morogoro. | Morogoro | 28,296,450.00 |
| 6 | Chama cha Viziwi Tanzania, Tawi la Mara P.O. Box 1013 Musoma | Advocacy strengthening among the community of people with disabilities. | Mara | 16,936,700.00 |
| 7 | Children, Youth and Family Support Trust (CHIYOFAST), P.O. Box 71283, Dar es Salaam | Empower community to participate in poverty eradication initiatives. | Dar es salaam | 34,411,000.00 |
| 8 | Community Concerns of Orphans and Development Association, P.O. Box 711, Njombe | Increase knowledge on land rights and ownership. | Iringa | 69,946,000.00 |
| 9 | Community Development and Relief Agency, P.O. Box 10636, Mwanza | Creating awareness to civil society groups on local government reform programme. | Mwanza | 104,961,900.00 |
| 10 | Human Development Trust, P.O. Box 65147, Dar es Salaam | Strengthening of youth groups and networks to participate in policy processes. | Dar es salaam | 34,680,000.00 |
| 11 | Jumuiya ya Uhifadhi wa Mazingira, P.O. Box 2576, Zanzibar Kusini Unguja | To educate the Southern Unguja community on the National forestry policy and laws. | Southern Unguja | 13,122,200.00 |
| 12 | Kasulu Initiatives and Development Trust Fund, P.O. Box 287, Kasulu | To educate farmers on the crop pest control law ("Batobato"- Cassava Bug) | Kigoma | 34,455,070.00 |
| 13 | Kibondo Environmental Management Association, P.O. Box 39 Kigoma | Educating the community on widows and women rights to property and land ownership. | Kigoma | 33,808,250.00 |
| 14 | Kijichi Beach Development Association, P.O. Box 41574, Dar es Salaam | Enhancing good governance to local government leaders and community members. | Dar es salaam | 33,635,,750.00 |
| 15 | Kikundi cha Mazingira Holili, P.O. Box 11 Himo, Moshi | Educating the community on the importance of good governance for sustainable development. | Kilimanjaro | 20,652,200.00 |
| 16 | KILUMPA, P.O. Box 313, Kyela | To fight against outdated values which hinder development and good governance. | Mbeya | 16,504,000.00 |
| 17 | Legal Services and Social Research Foundation, P.O. Box 5895, Dar es Salaam | Strengthening and capacity building to ward tribunals and ward development committees in Ilala district. | Dar es salaam | 34,270,900.00 |
| 18 | Life at Cross Roads Registered Trustees, P.O. Box 76124, Dar es Salaam | Integrated approach towards building youth to become responsible citizens. | Dar es salaam | 34,965,675.00 |
| 19 | Life Skills Association (LISA), P.O. Box 78303, Dar es Salaam | Strengthen the capacities of NGO's and CSO's in life skills facilitation. | Dar es salaam | 34,340,050.00 |
| 20 | Lumbesa Group, P.O. Box 4114 Dar es Salaam | Empowering the Kinondoni district communities on understanding Public expenditure for sustainable development. | Dar es salaam | 34,922,043.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 21 | Maji na Maendeleo Dodoma,<br>P.O. Box 311, Dodoma | Conduct training on National Water policy as related to MKUKUTA. | Dodoma | 17,152,896.00 |
| 22 | Makoye Resources and Technologies Agency,<br>P.O. Box 2002, Tabora | Creating awareness on children's and widows rights. | Tabora | 28,700,550.00 |
| 23 | Mategemeo Women Association,<br>P.O. Box 742, Arusha | Urban and rural youth education project in building youth rights. | Arusha | 32,912,880.00 |
| 24 | Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake Mkoa wa Ruvuma,<br>P.O. Box 88, Songea | Establish and strengthen women economic groups in Ruvuma. | Ruvuma | 69,999,950.00 |
| 25 | Mkolowony Development Agency Limited,<br>P.O. Box 283, Marangu, Moshi | Sensitize on National Strategy on Economic Growth and Poverty Reduction (MKUKUTA) | Kilimanjaro | 34,887,215.00 |
| 26 | Morogoro Paralegal Centre for Women and Children,<br>P.O. Box 6584, Morogoro | Awareness creation about the new Land laws for ward and village Land committees. | Morogoro | 34,813,900.00 |
| 27 | Muungano wa Vikundi vya Maendeleo Mzundu,<br>P.O. Box 38, Kabuku, Korogwe | Improving governance at community level by enhancing participation, transparency and accountability on different development issues. | Tanga | 27,117,500.00 |
| 28 | Mwela Theatre Group,<br>P.O. Box 42590, Dar es Salaam | Enlighten the community on good governance at grassroots' level. | Dar es salaam | 31,351,710.00 |
| 29 | Neighbours without Borders,<br>P.O. Box 238 Kigoma | Educating the community about land laws (Laws no. 4 and 5) of 1999 | Kigoma | 34,979,480.00 |
| 30 | Nenda Group,<br>P.O. Box 726, Songea | Education on proper diet to people living with HIV/AIDS. | Ruvuma | 22,447,100.00 |
| 31 | Network Against Female Genital Mutilation (NAFGEM)<br>P.O. Box 6413, Moshi | Promote studies and dissemination on to what extent women and children's rights are violated. | Kilimanjaro | 34,668,662.00 |
| 32 | Newala Development Foundation, (NDF),<br>P.O. Box 191, Newala | Training seminar on good governance to grassroots village leaders and NDF members. | Mtwara | 31,951,947.00 |
| 33 | Novelty Youth Centre,<br>P.O. Box 5551, Tanga | Capacity building to young girls on ways of reducing poverty in Tanga town. | Tanga | 34,994,883.00 |
| 34 | Organization for Youth, Community Rights and Development,<br>P.O. Box 5947, Dar es Salaam | Community engagement in Health System at Mkuranga District. | Pwani | 26,113,900.00 |
| 35 | Pensioners Union of Tanzania,<br>P.O. Box 71000, Dar es Salaam | Improving the living standard of pensioners and elderly people. | National | 18,389,000.00 |
| 36 | Relief to Development Society<br>P.O. Box 157, Kibondo | Enhancing labor force and capacity building to people living with HIV/AIDS | Kigoma | 35,000,000.00 |
| 37 | SAIPRO Trust Fund,<br>P.O. Box 1, Same | Citizens' participation in leadership and governance process. | Kilimanjaro | 83,976,965.00 |
| 38 | Songea Beekeeping Association,<br>S.L.P 591, Songea | Environmental education and improved beekeeping skills to Songea Beekeepers. | Ruvuma | 21,249,670.00 |
| 39 | Tanga Youth Development Association<br>P.O. Box 5344, Tanga | Participation of youth towards the implementation of the National Youth Development policy. | Tanga | 24,200,280.00 |
| 40 | Tanzania Arts Program,<br>P.O. Box 2067, Morogoro | Kids participatory theatre and sports against HIV/AIDS project. | Morogoro | 21,773,600.00 |
| 41 | Tanzania Cheshire Foundation,<br>P.O. Box 10269, Dar es Salaam | Stimulating disabled people in the community in order for them to know their rights. | Coast | 34,623,000.00 |
| 42 | Tanzania Mineral Mining Trust Fund,<br>P.O. Box 887, Songea | Capacity building to small scale miners and villagers on environmental conservation. | Ruvuma | 26,480,000.00 |
| 43 | Tanzania National Institute for the Blind,<br>P.O. Box 16454, Dar es Salaam | Enabling blind people to be self reliant. | National | 73,931,960.00 |
| 44 | Tanzania Water & Environmental Sanitation,<br>P.O. Box 71, Kibondo | Empowering the community on management of water schemes. | Kigoma | 34,914,600.00 |
| 45 | Tanzania Youth Exchange Network,<br>P.O. Box 95073, Dar es Salaam | Raising awareness on the importance of youths in the development process. | Dar es salaam | 32,800,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 46 | Tanzania Youth Self-Employed Development Association, P.O. Box 545, Njombe | Creating awareness on HIV/AIDS among groups of migrant labourers in tea plantations in Njombe district. | Iringa | 33,800,000.00 |
| 47 | TCCIA Songea Rural, P.O. Box 442, Songea | Provide education on business and entrepreneurship to small scale farmers and businessmen. | Ruvuma | 34,887,450.00 |
| 48 | The International Good Samaritan Mission (MIBOS) P.O. Box 501, Kigoma | Equal rights to access and own land for agricultural activities. | Kigoma | 34,990,700.00 |
| 49 | Tukolene Youth Development Centre, P.O. Box 43090, Dar es Salaam | Empowering Quran teachers with life skills education. | Dar es salaam | 34,965,000.00 |
| 50 | Tushirikiane Kupambana na UKIMWI Tanzania, P.O. Box 4, Tabora | Provide education on inheritance and human rights to widows and orphans. | Tabora | 28,285,550.00 |
| 51 | Umoja wa Vijana wa Kusaidiana na Kuelimishana Tegeta, P.O. Box 66615, Dar es Salaam | Education on effects of drug abuse in Kinondoni district. | Dar es salaam | 15,533,880.00 |
| 52 | Umoja wa Wawezeshaji wa Kioo, P.O. Box 1359, Kigoma | Educating the Ilagala community on good governance. | Kigoma | 24,494,600.00 |
| 53 | Umwema Group Morogoro, P.O. Box 1272, Morogoro | Sensitize the rural community on anti corruption initiatives at grassroots' level. | Morogoro | 64,008,000.00 |
| 54 | Unity for Disaster and Development Assistance, P.O. Box 867, Shinyanga | Capacity building for farmers and increasing food security. | Shinyanga | 22,248,600.00 |
| 55 | Unity in Diversity Foundation, P.O. Box 6404 Mbeya | Sensitizing and educating the community on their own rights. | Mbeya | 20,287,500.00 |
| 56 | Uprising Cultural Group, P.O. Box 912, Jang'ombe, Mjini Magharibi, Zanzibar | Build sustainable and peaceful families of fishing communities in Micheweni. | Northern Pemba | 7,054,500.00 |
| 57 | Vijana Vision Tanzania, P.O. Box 28099, Dar es Salaam | Training of the civil societies on the National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (MKUKUTA) | Pwani | 32,701,450.00 |
| 58 | Vuka Tanzania, P.O. Box 11460, Dar es Salaam | Community empowerment on orphans care. | Dar es salaam | 33,113,600.00 |
| 59 | Women Assistance Orphan Group, P.O. Box 628, Moshi | Advocacy for children rights as stipulated under UN conversion of April 2001 to the community. | National | 28,292,224.00 |
| 60 | Youth Advisory and Development Council P.O. Box 410, Shinyanga | Control and prevention of HIV/AIDS in Songwa ward community. | Shinyanga | 33,891,390.00 |

## Ruzuku Ndogo (RSG) –Novemba 2006

**Mnamo mwezi wa Novemba 2006, kamati ya utezi ya the Foundation inayohusika na kuchagua asasi zinazofaulu kupata ruzuku, imepitisha miradi yenye thamani ya shilingi milioni 172.6 kwa mashirika mbalimbali ya kiraia 35. Yafuatayo ni majina ya asasi zilizopata ruzuku hiyo ambazo utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwezi January 2007:-**

| Na | JINA LA SHIRIKA | MAELEZO YA MRADI KWA UFUPI | MKOA | KIASI KILICHITOLEWA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Association of Iringa High Quality Farmers Products Company Limited P.O Box 246, Iringa | Build capacity to farmers on entrepreneurship and the use of proper weighing measures on selling their crops. | Iringa | 5,000,000.00 |
| 2 | Birikau Farming and Fishing Cooperative Society P.O Box 183, Chake Chake, Pemba | Conduct training on environmental protection to the Kwale community. | South Pemba | 4,350,350.00 |
| 3 | Chama cha Kusaidia Watoto Yatima Makambako P.O Box 103, Makambako | Build sustainable strategies in helping orphans who are living in difficult conditions. | Iringa | 5,000,000.00 |
| 4 | Chama cha Maendeleo ya Wafugaji Purka P.O Box 17, Handeni | Conduct seminar on The National Environmental policy and law governing the Pastoralists. | Tanga | 4,999,800.00 |
| 5 | Chama cha Walemavu Tanzania, Tawi la Mbeya P.O Box 2361, Mbeya | Promote equal participation to people with disabilities in life reinforcement and community's wellbeing. | Mbeya | 5,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Chama cha Walimu Tanzania, Tawi la Songea Manispaa<br>P.O Box 1232; Songea | Provide education on HIV/AIDS to teachers of Songea municipal. | Ruvuma | 4,929,680.00 |
| 7 | Chemba Savings and Credit Cooperative Society Limited<br>P.O Box 1568, Iringa | Raising awareness to farmers on the National Policy for agriculture, and development of villages in life reinforcement. | Iringa | 4,974,790.00 |
| 8 | Community Development Support<br>P.O Box 129, Shinyanga | Raising awareness on children rights at grass root level. | Shinyanga | 4,999,800.00 |
| 9 | Environmental Conservation, Water Supply and AIDS Control Organization | Empowering street committees for improved performance in executing their daily responsibilities. | Dar es salaam | 4,989,500.00 |
| 10 | Family and Care of the Needs Group<br>P.O Box 2006, Shinyanga | Increasing understanding to the Ngokolo community on orphans and widows rights. | Shinyanga | 4,999,600.00 |
| 11 | Hope Farming Group<br>P.O Box 340, Urambo | Build capacity to widows and orphans in fighting for their basic rights. | Tabora | 4,973,600.00 |
| 12 | Jiendeleze Trust Fund<br>P.O Box 5057, Dodoma | Improve psychosocial support services for orphans and vulnerable children. | Dodoma | 4,962,550.00 |
| 13 | Jumuiya ya Matumaini – Hope and Care<br>P.O Box 188, Wete, Pemba | Education on the effects of drug abuse and HIV/AIDS in Wete district. | Pemba | 5,000,000.00 |
| 14 | Jumuiya ya Wafugaji, Wakulima na Mazingira ,<br>P.O Box 159, Zanzibar | Raising awareness on the National Policy for agriculture and pastoralism to farmers and pastoralists. | Kusini Unguja | 4,974,400.00 |
| 15 | Kawe Ridhika Shinda HIV/AIDS<br>P.O Box 60148, Dar es salaam | Community sensitization on the prevention and re-infection of HIV/AIDS and fighting against stigma to the people infected. | Dar es salaam | 5,000,000.00 |
| 16 | Kikundi cha Walemavu Makete<br>P.O Box 76, Makete | Educating the community on the needs and rights of people with disabilities. | Iringa | 4,782,440.00 |
| 17 | Kilombero High Quality Rice Growers Company Limited<br>P.O Box 454, Kilombero | Conserving and protecting the natural environment of Kilombero valley. | Morogoro | 4,999,800.00 |
| 18 | Kisinga Women Group<br>P.O Box 114, Makete | Educating the community on Land Act No. 4 and 5 of 1999. | Iringa | 5,000,000.00 |
| 19 | Kituo cha Maendeleo ya Utamaduni Ngerengere, P.O Box 484<br>Morogoro | Provide training to the community on the prevention of environmental destruction(pollution) | Morogoro | 4,776,650.00 |
| 20 | Mawengi Development Association<br>P.O Box 162, Ludewa | HIV/AIDS awareness among the youth and Local Government leaders. | Iringa | 4,996,550.00 |
| 21 | Mihovu United Group<br>P.O Box 1632, Morogoro | Education provision to Government leaders about transparency on the issues of financial public institutions. | Morogoro | 4,891,200.00 |
| 22 | Mtama Organization for Poverty Eradication<br>P.O Box 63, Lindi | Provide entrepreneurship skills to youth in Lindi district. | Lindi | 5,000,000.00 |
| 23 | Nzega Gospel Choir<br>P.O Box 335, Nzega | Train community leaders on Good governance at the grass root level. | Tabora | 4,994,100.00 |
| 24 | Plan Poverty Alleviation<br>P.O Box 874, Songea | Provide education on entrepreneurship to youths in streets and who have no proper place to live in. | Ruvuma | 4,724,650.00 |
| 25 | Save the Youth Development Association,<br>P.O Box 10752<br>Dar es salaam | Provide education on entrepreneurship to youths and leaders of Buguruni ward. | Dar es salaam | 5,000,000.00 |
| 26 | Society for Women and AIDS in Africa (SWAAT) Tanzania Branch, Morogoro rural,<br>P.O Box 762<br>Morogoro | Provide psychosocial skills to guardians of orphans and children living in difficult conditions. | Morogoro | 5,000,000.00 |
| 27 | Tabora Women Network Limited<br>P.O Box 693, Tabora | Community sensitization on raising awareness to women in fighting for their basic human rights. | Tabora | 4,999,995.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 28 | Tanzania 4H Organization<br>P.O Box 245, Himo, Moshi | Entrepreneurship training and Policy identification to youth in rural Moshi. | Kilimanjaro | 4,674,800.00 |
| 29 | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture<br>P.O Box 31, Namtumbo | Build capacity on the National Development Policy implementation of small industries and businesses to private sectors. | Ruvuma | 4,996,300.00 |
| 30 | Tanzania Peasants Rights Association<br>P.O Box 75965, Dar es salaam | Provide training to the Temeke district community on environmental protection. | Dar es salaam | 4,999,400.00 |
| 31 | Tanzania Volleyball Association<br>P.O Box 3868, Dar es salaam | Awareness creation among the youth on the Sports Development Policy. | Dar es salaam | 5,000,000.00 |
| 32 | Tupendane Group Himo<br>P.O Box 1, Himo | Provide education on Land Acts of 1999. | Kilimanjaro | 4,951,100.00 |
| 33 | Tuwajali Watoto Wasiojiweza na Yatima Community Centre<br>P.O Box 1621, Tabora | Awareness raising on the basic widows rights. | Tabora | 4,847,150.00 |
| 34 | Widem Youth Future Programme<br>P.O Box 28099, Kisarawe | Capacity building to youths on Entrepreneurship skills in Pwani region. | Pwani | 5,000,000.00 |
| 35 | Women Rights Action Group<br>P.O Box 471, Kigoma | Forest conservation and life reinforcement to the communities of Kigoma region. | Kigoma | 4,903,360.00 |

## Ruzuku Kubwa

**Mnamo mwishoni mwa mwaka 2006, kamati ya utezi ya the Foundation inayohusika na kuchagua asasi zinazofaulu kupata ruzuku, imepitisha miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.9 ya ruzuku kubwa kwa mashirika nane ya kiraia. Yafuatayo ni majina ya asasi zilizopata ruzuku hiyo::-**

| Na | JINA LA SHIRIKA | MAELEZO YA MRADI KWA UFUPI | MKOA | KIASI KILICHITOLEWA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Carpe Diem Ink | Increasing awareness of the National Pro-poor policies to the general public and development workers across the government and civil society through a published 6-monthly simplified policy review magazine | National | 300,000,000.00 |
| 2. | Concern for Development Initiatives in Africa (ForDIA) | Strengthening structures of governance at local government level for improving the quality of governance with a special focus of effectively reducing corruption. | National | 298,869,180.00 |
| 3. | International Trachoma Initiatives | Reducing the burden of trachoma and thus improving quality of life and social well being in 10 districts within Tanzania mainland. | National | 267,180,000.00 |
| 4. | Kilimanjaro NGOs Cluster (KINSHAI) | Promotion of Socio-Economic and Reproductive Health Rights of Women and Youth in Kilimanjaro Region. | Kilimanjaro | 299,384,371.00 |
| 5. | Mkombozi Centre for Street Childen | Protection of street and vulnerable children and young people by providing supporting and strengthening and advocating for community services in Moshi, Kilimanjaro and Arusha regions. | Kilimanjaro and Arusha | 299,253,938.00 |
| 6. | Social Action Trust Fund (SATF) | To build capacity of partner NGOs in order for them to enhance their knowledge on psychosocial skills delivery to orphans and vulnerable children. | National | 104,019,750.00 |
| 7. | Umoja wa Walemavu Zanzibar (UWZ) | To build capacity of persons with disabilities so as to enable them to be included in the mainstream of society development through improved quality of life and standard of living. | National | 100,000,000.00 |
| 8. | Youth Action Volunteers (YAV) | Contributing to the engagement and interaction between young men and women as health service users on one hand, policy makers and health service providers on the other hand. | Dar es Salaam and Pwani | 300,000,000.00 |
| | **Total amount committed** | | | **1,968,707,239.00** |

# `Sekta ya Biashara Iwajibike Kuleta Maendeleo ya Jamii'

Na Sitta Peter



sitta@thefoundation-tz.org

**UWAJIBIKAJI wa sekta ya biashara kwa jamii ni miongoni mwa njia zinazofaa katika kukusanya rasilimali zaidi kwa ajili ya kusaidia asasi za kiraia.**

Hayo yalielezwa wakati wa mkutano uliofanyika mwishoni mwa Novemba 2006, ambapo Menejimenti ya the Foundation na wadau wa maendeleo walipokutana kujadili maendeleo ya asasi hiyo.

Wadau hao walisema ikiwa sekta ya biashara itahamasishwa kuwajibika katika kuwasaidia watu wenye hali duni, rasilimali zitapatikana ndani ya jamii husika na kutakuwa na matumaini ya uendelevu wa asasi za kiraia na the Foundation.

Aidha ilisisitizwa kuwa sekta binafsi inapaswa kuhamasishwa kujijengea maadili na kuchangia katika maendeleo ya uchumi, huku ikiboresha hali ya maisha ya jumuiya inayowazunguka na jamii kwa ujumla, badala ya kujishughulisha kutafuta faida peke yake.

Hata hivyo, wadau hao walisema hatua hizo zitawezekana ikiwa Fthe oundation itayatangaza mafanikio ya huduma zake na ya asasi za kiraia, na hivyo walipendekeza kuwa ukusanyaji na uchapishaji wa taarifa za mafanikio ya asasi za kiraia ufanyike mara kwa mara.



*Baadhi ya Wabia wa Maendeleo katika Mkutano wa pamoja na the Foundation*

## PONGEZI

**The Foundation yampongeza Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Bi. Henny de Vries, na Afisa Ruzuku, Halima Dedengo, aliyeteuliwa kuwa Mkuu Mpya wa Wilaya ya Mpwapwa**



Bi. Dendego Mkuu Mpya wa Wilaya ya Mpwapwa



Bi. Henny de Vries Mwenyekiti wa zamani wa Bodi ya the Foundation

## TANZIA

Mwishoni mwa mwaka 2006, the Foundation for Civil Society ilipoteza mmoja wa wafanyakazi wake, Hilda Mvinile, ambaye alikuwa Msaidizi wa Utawala. Alifariki Desemba 7, 2006 kutokana na matatizo yanayohusiana na kushuka kwa shinikizo la damu.



Hilda alikuwa na uwezo mkubwa wa kufanya kazi au kushirikiana na watu wa tabia na ngazi tofauti, bila mgogoro. Wanaomfahamu wamemwelezea kuwa mtu mwepesi kusamehe, mpole, mcheshi na mwenye bidii ya kazi. Alipenda kujifunza na alionesha moyo wa kufanya kazi katika timu kwa vitendo. Ni sifa hizo zilizomwezesha kuwa "Mfanyakazi bora" wa the Foundation kwa mwaka 2005.

**Mungu aipumzishe roho yake kwa amani milele**

THE FOUNDATION
for Civil Society

# Ratiba ya ruzuku kutoka The Foundation - 2007

| Aina za Ruzuku | Kiwango cha Juu kwa Mwaka | Kiwango cha Juu cha muda wa ruzuku | Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi | Mwombaji atajulishwa katika muda wa | Kama imekubaliwa fedha zitatolewa katika muda wa |
|---|---|---|---|---|---|
| Ruzuku kubwa | Shs 100 Milioni | Miaka 3 | Muda wowote | Majuma 16 | Majuma 24 |
| Ruzuku ya Kati | Shs 35 Milioni | Miaka 3 | Februari 1, Juni 1, Oktoba 1 | Majuma 8 | Majuma 16 |
| Ruzuku Ndogondogo | Shs 5 Milioni | Mwaka 1 | Aprili 1, Julai 1, Septemba 1, Novemba 1 | Majuma 8 | Majuma 16 |
| Ruzuku ya Usajili | Shs 200 elfu | Mara moja | Muda wowote | Majuma 8 | Majuma 16 |

**Kupata ruzuku ni haki, usikubali kutoa au kupokea rushwa.**

*Kwa habari zaidi, wasiliana nasi:*

**The Foundation for Civil Society**
Haidery Plaza, Ghorofa ya 5, Mtaa wa Upanga/Kisutu. S.L.P. 7192, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2138530, 2138531, 2138532. Faksi: +255 22 2138533
Barua pepe: information@thefoundation-tz.org Tovuti: www.foundation.tz.org